TOLEO NO.63

# Khilafah

NDIO SULUHISHO

(DHUL-HIJJAH 1446 HIJIRIA —JUNI 2025 MILADIA) ( Bei Tsh 2,000/= - Ksh 100/=)

## MASLAHI CHANZO CHA 'HAMA HAMA' KATIKA VYAMA

Katika siku za karibuni kumekua na wimbi kubwa la baadhi ya viongozi na wanachama wa Chadema kuhama katika chama hicho na kujiunga na kujiunga na **Chama cha Ukombozi wa Umma (CHAUMMA)**. Haya yanajiri baada ya mchuano wa uchaguzi wa kambi mbili ndani ya Chadema, yaani kambi ya aliyekuwa Mwenyekiti Freeman Mbowe na mwenyekiti mpya wa sasa Tundu Lissu.

Huko nyuma tulishuhudia hama hama kama hii kwa kuhama watu mashuhuri kama Zitto Kabwe kutoka Chadema na kuanzisha chama cha ACT-Wazalendo mwaka 2014, Edward Lowasa ndani yam waka 2015 akitokea CCM kwenda Chadema, na wengi ndani ya mwaka 2018 kama Mwita Waitara aliyekuwa mbunge wa Chadema jimbo la Ubungo, Mwenyekiti wa Kamati ya Uongozi ya Chama cha CUF maarufu kama Chama Cha Wananchi bwana Julius Mtatiro nk.

Vituko hivi vya 'hama hama' katika demokrasia si jambo la kushangaza, kutokana na nidhamu hiyo inayotokana na aqida kituko na ya kusha




ngaza ya 'usekula'.

Demokrasia ni nidhamu iliyojengwa juu ya kipimo kimoja tu cha hatari katika matendo, nacho ni 'maslahi'. Yaani mtu hutenda jambo au huacha kutenda ikiwa kuna maslahi. Si ajabu kwa mwanademokrasia awe kiongozi au mwengine yoyote kutenda lolote litakalodhamini maslahi yake. Mara ngapi tunashuhudia wanachama na viongozi wa chama fulani kuhama na kujiunga na chama kingine kufuata maslahi yao, hata kama chama wanachohamia kimejaa mapungufu ambayo awali walionekana kuyakemea.

Hivyo, mwanasiasa ndani ya mchakato wa siasa za kidemokrasia daima yuko mbioni kutafuta maslahi tu. Anayebakia katika chama ni kwa sababu kuna maslahi, na anayehama ni kwa sababu maslahi yameondoka, yamepungua au anakwenda kwenye maslahi zaidi. Katika hali hiyo ni jambo la kawaida kwa wanasiasa wa kidemokrasia kuuza hata kinachoitwa misimamo ya kisiasa kufikia malengo ya kimaslahi. Ni vipi mwanasiasa huyo kama kuna fursa ya kudhamini au kulinda maslahi yake zaidi aiwache? Na vipi mwanasiasa wa aina hiyo abakie katika chama ikiwa maslahi yake yako hatarini au yamekosekana?

Kwa msingi huo wa maslahi, vyama vyote vya kidemokrasia havipo kutetea au kupigania ustawi wa wananchi, bali ni vitega uchumi vya wanasiasa, amma kwa kula ruzuku ambayo ni mali ya Ummah, kupora fedha za miradi, kutarajia uteuzi, kutafuna misaada ya wakoloni, kula michango ya wafadhili matajiri, ya wanachama nk.

**Inaendelea Uk. 7**

**Yaliyomo :**


- **Ibada ya kuchinja na ukombozi wa Gaza- uk.2**
- **Funzo la uchaguzi wa Papa- uk.3**
- **Jee Mtume SAAW alirogwa? -uk.4**
- **Kufukuzwa washirikina Mji Mtukufu-uk.5**
- **Matukio ya Dhulhijjah uk. 7**




# IBADA YA KUCHINJA IWE CHACHU KUIKOMBOA GAZA NA UMMA KWA JUMLA

Tukiwa ndani ya masiku matukufu ya Dhulhijja, siku chache zijazo tutakuwa katika Siku kuu kubwa ya Eid-al adhha. Siku kuu hii ya kuchinja inafungamanishwa na ibada kubwa ya muhanga wa baba wa Mitume Nabii Ibrahim As. alipodhamiria kutekeleza amri ya Mola wake kwa kumtoa muhanga mtoto wake mdogo Nabii Ismail As.

Tukio hili kubwa la aina yake katika tariikh ya ubinadamu ambalo limebakia kuwa Sunna

kwetu kuchinja mnyama katika siku kuu hii linapaswa kutupa msukumo na msimamo wa dhati

wa moyo wa kujitolea muhanga katika kulinda imani, maisha, matukufu yetu nk.

Umma wetu wa Kiislamu lazima utanabahi kuwa hakuna wakati ambao muhanga unahitajika

zaidi kuliko wakati huu. Tumeishi kwa miaka 104 sasa bila ya utawala wetu wa dola ya

Khilafah baada ya kuangushwa na makafiri kwa msaada wa wanafiki.

Baada ya kuondoshwa kinga hiyo (dola ya Khilafah) Umma wetu umesambaratika na

kuparaganyika kama kondoo asiyekuwa na mchunga, na umesibiwa na unyonge na udhalili kama kiwindwa kilichozingirwa na simba. Na kamwe Umma wetu haukupata tena siku ya utulivu na amani kwa kipindi chote, kama tunayoshuhudia sasa ya mauaji ya halaiki ndani ya Gaza.



Tukio la dhulma, unyama na ukatili wa Israili ndani ya Gaza ni katika kielelezo kisicho na shaka juu ya uhitaji wa dhati wa kila mmoja katika Umma wetu kujitolea muhanga kwa uwezo na nafasi yake katika sharia.

Wanavyuoni watumie athari, ushawishi wa kielimu, mimbari na majukwaa yao kukemea kwa

nguvu na kwa ukali watawala vibaraka katika ulimwengu wa Kiislamu juu ya khiyana na usaliti wao wa wazi wa kuwaacha mkono watu wa Gaza, na kusaidia kwao makafiri kwa hali na mali dhidi ya Waislamu wa Gaza. Kama yanayotendwa na Misri, Jordan kwa kufunga mipaka, au Uturuki inavyoshirikiana na Israili katika biashara. Bila ya kutaja Saudia, Qatar n Falme za Kiarabu walivyomzawadia Trump matrilioni ya fedha za Umma ili aendelee kuwapa Mayahudi nguvu zaidi za kuangamiza Waislamu wa Gaza.

Aidha, wanazuoni wapaze sauti zao kielimu kuwakumbusha majeshi katika ulimwengu wa Kiislamu juu ya hukmu ya kisharia ya kuingilia kijeshi mara moja kuikomboa Gaza na kuwakomboa wanawake, watoto na madhaifu ambao damu yao imeshangamia kwa maelfu

Wanajeshi nao katika nchi kubwa za Waislamu hususan zinazopakana na Israili watoe muhanga nao kwa kukikata minyororo ya vibaraka watawala kuitikia mwito wa Allah Taala wa kutuma vikosi vyao kuikomboa Gaza na Masjid Aqswa kwa jihadi.

Na Umma jumla wa Kiislamu nao kwa upande wake, nao haupaswi kuwa nyuma katika jambo

hili la muhanga kwa kupaza sauti dhidi ya dhulma na uovu wa mayahudi na washirika wake.

Bali unapaswa kuwaharakisha kuwaonesha majeshi katika ulimwengu wa Kiislamu kwamba

hawako peke yao lau watasimama kuitetea Gaza nk.

Kwa kuwa tunakaribia katika Eid-al adhha, tunachukua fursa hii adhimu kuutakia Umma wetu

mashariki na magharibi kila la kheri kwa Sikuu hii kubwa. Hata hivyo, tunatoa angalizo kwamba ibada ya kuchinja isiwache athari ya kujaza ladha tamu ya nyama mdomoni mwetu na kujaza matumbo yetu tu, bali iwe chachu ya mazingatio ya kujitolea muhanga na kuufanyia kazi ili kukomboa Umma wetu.

**Mhariri**

**01 Dhul-Hijjah 1446 H**

**29/04/2025 M**

***jukwalakhilafah@gmail.com***

## MAFUNZO KUFUATIA KUCHAGULIWA KWA PAPA MPYA

Tarehe 8 Mei 2025 ulimwengu ulishuhudia kuchaguliwa kwa Papa Leo (Robert Francis Prevost) kama Kiongozi mkuu wa Kanisa Katoliki duniani, Kanisa ambalo ndiyo kielelezo cha dini ya Ukristo ulimwenguni. Papa Leo alichaguliwa takribani siku 17 tangu kufariki kwa mtangulizi wake Papa Francis (Jorge Mario Bergoglio) aliyefariki dunia..

Matukio haya kwa pamoja yanatupa mazingatio kadhaa katika maisha yetu ya hapa ulimwenguni ikiwemo unyeti wa kiongozi katika jamii.

Jamii yeyote haiwezi kusonga mbele bila ya kiongozi atakayewapa dira wafuasi wa jamii hiyo.

Kwa upande wa pili, kukosekana kwa uongozi hufanya uendeshaji wa mambo kutokuwa madhubuti na kukosa tija.

Ukweli ni kwamba Papa ni kiongozi dhaifu mno kwa kuwa ni kiongozi wa kiroho tu. Hii ni kwa sababu Ukristo pia ni dini dhaifu inayojifunga na mabo ya kiroho tu (spiritual religion) na si dini ya kimfumo (ideological religion). Kwa maana ya kwamba haina masuluhisho katika sekta za maisha ya mwanadamu, zaidi ya vijiibada fulani fulani tu.

Kwa kuwa ili dini iwe ya kimfumo hulazimu iwe na itikadi, kisha itikadi hiyo izalishe sheria na nidhamu zote za maisha duniani.

Kwa hivyo, ukishachagua itikadi hiyo, basi umechagua sharia, kanuni na taratibu za maisha yote ya mwanadamu kutoka ndani ya mfumo huo



husika. Ukristo ni Dini ya kiroho tu kwa kuwa itikadi yake haijazaa sharia, nidhamu wala taratibu za kimaisha kama sera za uchumi, kisiasa na kijamii nk. Hata hivyo. licha ya udhaifu huu wa Ukristo bado wakristo hawajakubali kukaa hata muda mfupi bila ya kuwa na kiongozi.

Na mara baada tu ya kifo cha Papa Francis kwa mujibu wa taratibu zao za uchaguzi wamefanya haraka kumchagua Papa mwengine mahala pake.

Uislamu ni mfumo kamili wa maisha ya binadamu ulioletwa kutoka kwa Muumba, na itikadi yake imezalisha sheria na nidhamu za kimaisha katika nyanja zote sawa sawa iwe ni siasa, uchumi na jamii.

Uislamu unatoa masuluhisho ya matatizo yote ya binadamu katika sheria zake safi na fafanuzi.

Kwahiyo, Uislamu haukuacha suala la uongozi katika Ummah bila ufafanuzi bali umelielezea na kulisisitiza kuwa ni jambo la wajibu kwa Ummah wa Kiislamu, kuwa na kiongozi wao wa mmoja kiulimwengu (Khalifah)

Cha kushangaza wakristo ambao dini yao haina nidhamu ya Uongozi na Utawala (political system) wanafanya hima ya kuweka kiongozi wao, ilhali kwa masikitiko makubwa Waislamu wenye dini ya mfumo kamili wenye nidhamu ya uongozi na utawala kwa bahati mbaya mpaka leo hii kwa miaka 101 hawana kiongozi wao yaani Khalifah.

Uislamu umelifanya suala la uongozi na utawala ni jambo kubwa nyeti na la lazima ambalo halipaswi kuzembewa, kiasi ambacho Mtume (SAAW)akasema Muislamu ambaye atakufa bila ya kuchagua kiongozi/ mtawalakwa kutoa kiapo cha utiifu cha baiya atakuwa amekufa kifo cha kabla ya Uislamu, yaani kifo cha Kijahiliya.

Anasema Mtume(SAW) kuwa:

من مات بغير امام مات ميتة جاهلية

"Yeyote atakayekufa bila ya kuwa na Imamu (Khalifah) atakukufa kifo cha kijahiliya" (Ahmad, Hakim, nk)

Hii inaonesha uwajibu na umuhimu mkubwa wa kuwa na kiongozi mtawala wa kiulimwengu kwa Waislamu.

Mtawala ambaye atasimamia ute -kelezaji wa sheria za Mwenyezi Mungu hapa duniani na kubeba ujumbe wa Uislamu dunia nzima.

Jukumu hili la Umma kuwa na kiongozi/Khalifah litusukume kufanya kazi ya ulinganizi usiku na mchana ili Ummah wetu utokane na dhima ya kifo kibaya cha Kijahiliya.

Kwani Umma wetu umekosa kiongozi huyo na umebakia yatima bila ya mchunga na hauna kinga tangu kuvunjwa kwa njama na hila za makafiri na vibaraka kwa dola ya mwisho ya Kiislamu, KhilafaUthmania mwaka 1924 huko Istanbul.

## JEE MTUME (SAAW) ALIROGWA ?

**Swali:**

Je Inawezekana kuwa Mtume ( SAAW ) alirogwa? Mpaka alikuwa kama anavyopokea Bi Aisha, kwamba yeye Mtume (SAAW) anadhani kwamba kafikiwa na kitu ilihali hajafikiwa na kitu chochote, mpaka alikuwa (Mtume) anadhani kuwa amewaingilia wake na hali ya kuwa hajawaingilia.

**Jibu:**

Hili tamko la Hadithi na yale yaliopokelewa katika kauli:

***Bi Aisha (Allah awe Radhi naye) amesema : Amemroga Mtume (SAAW ) mtu kutoka kabila la Bani Zuraiq,anaeitwa Labid Bin Al-a'aswam, mpaka alikuwa Mtume (SAAW) akidhanishiwa kuwa kafanya kitu na kumbe hakufanya kitu' (Bukhari)***

***( Na katika mapokezi mengine ya Bukhari Bi Aisha (ra) amesema: "Mpaka alikuwa (Mtume SAAW) anaona kana kwamba amewaingilia wake zake na hali ya kuwa hajawaingilia"***

Na inawezekana kufupisha shubha zilizopo katika Hadithi hii katika mambo matatu:

**Moja:** Kwamba Hadithi hii ijapokuwa kaipokea Bukhari na Muslim, hii ni Hadithi ahadi, haichukuliwi katika mambo ya Itikadi. Na pia haichukuliwi katika jambo la kuhifadhiwa Mtume (SAAW) na kuathirika na uchawi katika akili yake. Na itikadi haichukui katika kuthibitisha isipokuwa kwa yaqini kama 'Hadithi Mutawatir,' na wala haitoshi Hadithi Dhanii katika hilo.



**Pili:** Hakika Hadithi hii inapingana na Qur'ani ambayo ni Mutawatir na Yakini, katika kukanusha kurogwa Mtume (SAAW). Qur'an imewakosoa washirikina na kuwafedhehi kwa kumnasibisha Mtume (SAAW) na kurogwa. Amesema Allah :

وقال الظالمون إن تتبعون إلا رجلا مسحورا

انظر كيف ضربوا لك الأمثال فضلوا فلا * يستطيعون سبيلا

***"Na Madhalimu wakasema "Nyinyi hamumfuati ila mtu aliyerogwa". "Tazama jinsi wanavyokupigia mifano (isiyokuelekea), basi wamepotea wala hawataweza (kushika) njia ilionyooka.*** **(TMQ 25 : 8-9 )**

Na anasema tena:

{ نحن أعلم بما يستمعون به إذ يستمعون إليك وإذ هم نجوى إذ يقول الظالمون إن تتبعون إلا رجلا مسحورا * انظر كيف ضربوا لك الأمثال فضلوا فلا يستطيعون سبيلا }

***"Tunajua sana sababu wanayosikilizia, wanapokusikiliza, na wanaponong'ona na kusema hao madhalimu, (kuwaambia Waislamu ili kuwapoteza) "Nyinyi hamumfuati isipokuwa mtu aliyerogwa".***

***Tazama jinsi wanavyokupigia mifano (ya uwongo, mara amerogwa, mara muongo, nk) Basi wakapotea, na hawawezi kupata njia (ya kuwapelekea katika haki)*** **[TMQ 17 : 47-48]**

Kwamba lau ingefaa kwa Mtume ( SAAW ) adhani kwamba kafanya kitu, kumbe hajafanya kitu, basi ingefaa pia adhani kwamba kashukiwa na kitu ( Wahyi ) kumbe hajashukiwa na chochote kile, au adhani kuwa kafikisha ujumbe fulani kumbe hajafikisha chochote, na hilo ni jambo muhali katika haki ya Mtume (SAAW), kwani linapingana na *'isma* (kuhifadhiwa kwake) katika ujumbe na kufikisha.

**Tatu:** Japo wapo walioithibitisha Hadithi hii na wakasema kuwa ni hoja Hadithi ahadi katika Itikadi, na wakatafsiri kule kurogwa kwa Mtume (SAAW) ni kurogwa kimwili pasina akili yake. Kauli hizi hazina msingi wowote wa kiakili wala kisheria na hazitegemewi na sisi. Msimamo wetu ni kutokuchukua Hadithi Ahadi katika mambo ya itikadi, na Allah ndio Mjuzi.

Anasema Sayyid Qutb –Allah Amrehemu – katika kitabu

**Inaendelea uk ….6**

## QUR,AN YAWAFUKUZA WASHIRIKINA KATIKA ARDHI TUKUFU LAKINI VIBARAKA WAWAPOKEA KWA HESHIMA

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوٓاْ إِنَّمَا ٱلْمُشْرِكُونَ نَجَسٌ فَلَا يَقْرَبُواْ ٱلْمَسْجِدَ ٱلْحَرَامَ بَعْدَ عَامِهِمْ هَٰذَا ۚ وَإِنْ خِفْتُمْ عَيْلَةً فَسَوْفَ يُغْنِيكُمُ ٱللَّهُ مِن فَضْلِهِۦٓ إِن شَآءَ ۚ إِنَّ ٱللَّهَ عَلِيمٌ حَكِيمٌ

Enyi Mlioamini! Hakika washirikina ni najisi. Basi wasiikaribie Msikiti Mtakatifu baada ya mwaka wao huu. Na mkikhofia umasikini, basi Mwenyezi Mungu atakutajirisheni kwa fadhila Yake ikiwa Atapenda. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi, Mwenye hikima." (At-Tawbah : 28)

Aya hizi zilishuka mwezi wa DhulHijja mwaka 9 Hijria. Hijja hii Mtume (SAAW) hakushiriki bali akiwa kama kiongozi alimchagua Saydna Abubakar ra. asimamie ibada hiyo. Hata hivyo, baada ya kushuka aya hizi Mtume (SAAW) alimtuma mjumbe maalumu Saydna Ally bin Abi Twalib aende Makka kufikisha agizo na tangazo hili zito.

Agizo katika aya hizi ni kuwapiga washirikina marufuku katika ardhi tukufu ya Makka pamoja na kuukaribia msikiti mtukufu wa Makka
Kisha badae ufafanuzi wa agizo ukaendela kupitia maagizo ya Mtume (SAAW) na kutanuka katazo hili la marufuku kwa washirikina wote katika eneo zima la Bara la Arabu kama alivyosema :
لَأُخْرِجَنَّ الْيَهُودَ وَالنَّصَارَى مِنْ جَزِيرَةِ الْعَرَبِ حَتَّى لَا أَدَعَ فِيهَا إِلَّا مُسْلِمًا
رواه مسلم، حديث رقم: 1767
"Hakika nitawatoa Mayahudi na Manaswara katika Bara Arabu mpaka nisimuache yeyote humo isipokuwa Muislamu" (Muslim).

Hapana shaka yoyote kwamba Uislamu hauna chuki na asiyekuwa Muislamu kwa sababu ya kuto kuwa kwake Muislamu ndio maana ukawa haumlazimishi mtu kusilimu kwa nguvu. Lakini Uislamu una maeneo yake maalumu hauruhusu dini zaidi ya Uislamu.
Na jambo hili si aibu wala ajabu.
Kwa mfano, leo Vatican hawawezi kuruhusu kujenga msikiti katika eneo lao kwani kwao wao wana amini eneo hilo ni ardhi yao tukufu, japo ni mawazo yao tu ya kupandikizwa. Kwani kwa jambo hilo walau lingeonekana kuwa na mashiko lau wangedai ardhi aliyozaliwa na kuishi Yesu hata kama ingekuwa si kweli.

Tukilizingatia tangazo hilo la Surat Tawba utaona ni kwa kiasi gani Umma wa Kiislamu leo ulivyotumbukizwa katika uduni na watawala vibaraka, Trump adui mkubwa wa Waislamu, Uislamu na binadamu badala ya kutimuliwa na kutokaribishwa katika miji ya Kiislamu anapewa heshima, hadhi kubwa na vibaraka walio kalia ardhi za Arabuni. Na sio tu kupewa heshima na hadhi bali anazawadiwa 5.4 Trilioni katika fedha za Umma. Aibu ya kiasi gani, mpaka makafiri wanatoa kebehi !!
Pesa ambazo zingeweza kufuta umasikini wa Waislamu wote duniani.
Mtume (SAAW) aliwatimua mapema sana mayahudi wote waliokuwa wakiishi Arabuni hasa karibu na Madina kutokana na uchafu wao, khiyana na uadui wao dhidi ya Waislamu. Miongoni mwao ni mayahudi wa Bani Nadhir na Banuu Qainuqaa
Amma mayahudi wa Banii Quraidha walibakia kwa muda, kwa bahati mbaya waliendendela uovu bila kupata mazingati kwa yaliyowafika wenzao.
Wakati Mtume (SAAW) amezingiwa katika Vita vya Ahzaab na washirikina wote wa Arabuni wakitaka kuuwa, kuchinja Waislamu wote wa Madina na kuangusha dola ya Kiislamu ili wamalize kabisa Uislamu na Waislamu. Katika hali kama hiyo mayahudi wa Banii Quraidha walivunja mkataba na kumsaliti Mtume (SAAW) kwa kushirikiana na washirikina kwa kufanya hujuma kwa ndani dhidi ya Waislamu. Ili Waislamu wachinwje ndani na nje.
Allah SWT. Alipoleta ushindi wake kwa Waislamu kwa njia ya muujiza, Bani Quraidha hawakustahiki adhabu yoyoyte zaidi ya kifo, kwani walichokifanya ni zaidi ya uhaini usaliti kwa dola na Waislamu.
Mtume (SAAW) akatoa agizo Bani Quraidha wote wauliwe ili fundishi kwa wengine
Leo Trump anayeendesha na kusimamia kuchinjwa kwa Waislamu ndani ya Palestina jumla hususan Gaza badala ya kutimuliwa anakaribishwa kwa heshima na taadhima, vibaraka wakijivua dini,heshma ya kibinadamu hata gherra ya kiarabu wkawapanga foleni wake zao na banati zao wakinengua mbele ya Trump ili aridhike na afurahi. Msiba wa kiasi gani huu??

## Kurogwa kwa Mtume (SAAW) *kutoka uk .4*

chake cha Fii Dhilalil-Qur'an akitafsiri Suratil-Falaq : **"Na shari ya wale wanaopuliza mafundoni…"** "Wanaopuliza katika mafundo ni wachawi wanaeneza ubaya kwa njia ya kuhadaa hisia na kuhadaa mishipa, na wao wanafunga fundo kwenye uzi au kitambaa (leso) na wanapulizia humo kama kuiga uigaji wa kiuchawi na kuingiza athari kwenye nafsi na kuathiri hisia!

Na uchawi haubadilishi tabia ya vitu, na wala hauleti hakika nyingine ya kitu, lakini huleta dhana katika hisia kama anavyotaka mchawi.

Na huu ndio uchawi kama ulivyoelezwa na Qur'an katika kisa cha Nabii Mussa As. katika Surat Twaha, ulionekana kwa watu miongoni mwao Musa As – kwamba fimbo zinatembea, mpaka kufikia kiwango cha kuingiza khofu katika nafsi ya Musa As. na kama hivi kiukweli fimbo zao hazikugeuka kuwa nyoka wa kiukweli mpaka ilipomjia ithibati. Kisha hakika na ukweli ukawa wazi pale ilipogeuka fimbo ya Mussa As. kiukweli ikawa nyoka, ikameza zile kamba na fimbo zilizogeuzwa nyoka kiuwongo na wachawi.

Hii ndio tabia ya wachawi, na kwa tabia hii wanawaathiri watu na wanapata hisia kwa mujibu wa vitendo vyao, hisia ambazo zinawatisha, kuwaudhi na kuwaelekeza mwelekeo wanaoutaka wachawi. Na kwa kiwango hiki tunasimama katika kufahamu tabia ya uchawi na kupuliza katika fundo.. Nayo ni shari ya kujilinda kwayo kwa Allah Taala na kuelekea Kwake kwa ulinzi.

Kwa hakika ni maarufu kuwa zimepokelewa Riwaya – baadhi yake ni sahihi, lakini hazifikii kiwango cha Mutawatir kuwa Labid Bin A'aswam Myahudi alimroga Mtume (SAAW).

Hata hivyo, mapokezi yote haya yanakhalifu msingi wa kuhifadhiwa Mtume (SAAW) kutokufanya makosa katika vitendo na kufikisha, na riwaya hizo zinagongana na itikadi ya Kiislamu inayotufundisha kuwa kila kitendo katika vitendo vyake Mtume (SAAW) na kila kauli katika kauli zake ni Sunnah na ni Sharia.

Na na pia riwaya hizo zinagongana na Qur'ani ambayo inakanusha kuwa Mtume (SAAW) karogwa, na inawakadhibisha washirikina katika madai yao hayo ya uongo. (ya kurogwa Mtume SAAW).

Kutokana na hayo, Hadithi hizi zinawekwa mbali… kwa kuwa Hadithi ahadi hazichukuliwi katika mambo ya itikadi. Na marejeo ni Qur'ani, na kuja kitu kikiwa Mutawatir ni sharti la kukubalika Hadithi katika Misingi ya Itikadi.

Kwa bahati mbaya mapokezi ya Hadithi hizi (zinazosema Mtume karogwa) sio Mutawatir. Bali pia kushuka kwa sura mbili (anazonasibishiwa Mtume kuwa kinga ya kurogwa) katika mji wa Makkah ni kauli yenye nguvu. Jambo hilo linadhoofisha msingi wa mapokezi ya Riwaya hizo.

**Ndugu yenu Sheikh Ata bin Khalil Abu Rashta**

**(Allah Amrehemu)**

**Amiri wa Hizb ut Tahrir**




**Tunawatakia Umma wa Kiislamu kila la Kheri katika Eid hii kubwa**

**EID UL-UDHHIYA**

## Matukio ya Dhul Hijjah

**1**. Kusilimu kwa Hamza na Umar RA. (Mwaka wa 6 wa Utume)

2. Baayah ya Kwanza (Mwaka wa 11 wa Utume)

3.Baayah ya Pili (Mwaka wa 13 wa Utume)

4. Ghazwa ya Assawiq (Mwaka wa 2 H baada ya vita vya Badr)

5.Ndoa ya Bi Fatma ra. (binti wa Mtume SAAW) mwaka 2 H)

6.Ghazwa ya Abdullah bin Atiq (Mwaka wa 4H.)

7. Ghazwa ya Ibn Abil Awja (Mwaka wa 7AH.)

8. Kutangazwa rasmi msimamo wa Surat Tawba wa kufukuzwa Mushrikina Makka. (Mwaka wa 9AH.

9.Hijjatul-Wadaa (9 Dhulhijjah Mwaka wa 10 AH.)

10. Siku ya Eid ul Udhiya (10 DhulHijjah)

11Masiku ya Tashriiq (tarehe 11 - 13Dhulhijja)

12.Kujeruhiwa vibaya (hadi kifo chake) Umar RA. (Mwaka wa 23H.)

13.Kupewa Baayah Ali bin Abi Twalib RA. (18 Ijumaa Mwaka wa 35 H)

15. Kuibuka kwa Vita vya Siffin (Mwaka wa 36H.)

## *Hama hama vyama.. Kutoka uk 1.*

Hili kimaumbile linapelekea kukosekana utulivu na kupatikana kuhama hama na migogoro isiyokwisha katika vyama hivi.

Aidha, siasa chini ya ubepari imegeuzwa kuwa ajira kama ajira nyengine, tena ajira kubwa. Kwa hivyo kila mmoja anaiangalia kwa jicho hilo. Ndio mana hata wataalamu wa fani mbali mbali wameachana na fani zao na kujitosa katika siasa kwa kuwa kuna fungu nono la maslahi.

Zaidi ya hayo demokrasia haina thamani ya kiroho, ya mtu kutenda kwa kutarajia malipo kwa Muumba, wala haina dhana ya kweli ya muhanga licha ya uwongo wa wanasiasa kujionesha wanajitolea muhanga katika kutetea na kuwatumikia raia. Kwa kuwa muhanga wa kweli ni ule unaofungamana na imani ya Muumba kwa kutarajia malipo kutoka kwake. Muhanga mkubwa wa wanademokrasia unalenga kukifikia kitu kimoja tu, nacho ni maslahi na sio jenginelo.

Mwisho, nidhamu ya kidemokrasia inashikilia fikra chafu za Machieveli zinazohubiri msimamo usemao: 'njia yoyote ni halali ikiwa itakufikisha kwenye lengo'. Katika demokrasia na waumini wake wanaweza kuwa vigeu geu au kutenda chochote hata kiwe na madhara kiasi gani ili kufikia maslahi wanayodhamiria. 'Hama hama' ni katika njia wanayoitumia wanademokrasia kuyafikia malengo yao ya maslahi

Kwa maumbile hayo ya demokrasia tuliyotaja, ni wazi nidhamu hiyo haiwezi kuepuka migogoro, 'hama hama' na husuma zisizokwisha ndani ya vyama vyake.

Aidha, tabia hizo huifanya nidhamu hiyo kuwa ni nidhamu tete, inayokosa nishati, isiyo na msimamo na iko mbali na kujitolea muhanga.

Basi yamtosha kila mtu makini na mwenye nia njema ya kuleta mageuzi ya kweli kujiepusha mbali kushiriki au kuunga mkono mchakato wa uwongo wa kidemokrasia. Na badala yake kushika njia/ manhaj sahihi ya Kiislamu ya mageuzi kama alivyofundisha Mtume (SAAW)

Na kwa wasiokuwa Waislamu muda umefika kwa wao kutafiti mfumo mbadala wa Kiislamu na njia yake ya mageuzi, kisha wasilimu na kujitenga na ubepari mfumo muovu, dhaifu na tete ambao watu huona kana kwamba wameshikilia kitu imara kumbe ni udanganyifu mtupu.

مَثَلُ الَّذِينَ اتَّخَذُوا مِنْ دُونِ اللَّهِ أَوْلِيَاءَ كَمَثَلِ الْعَنْكَبُوتِ اتَّخَذَتْ بَيْتًا وَإِنَّ أَوْهَنَ الْبُيُوتِ لَبَيْتُ الْعَنْكَبُوتِ لَوْ كَانُوا يَعْلَمُونَ

*"Mfano wa waliowafanya walinzi (wasimamizi wa mambo yao) badala ya Mwenyezi Mungu ni mfano wa buibui anavyojifanyia nyumba. Na hakika nyumba dhaifu mno kuliko zote ni nyumba ya buibui laiti wangelijua "*(29: 41)

**USIKOSE KUSOMA JARIDA LAKO LA KHILAFAH KILA MWEZI**

# HIJJA ITUSUKUME KUIKOMBOA GAZA




**Pichani:**

Wanaharakati wa Hizb ut Tahrir Tanzania wakiwa kwenye kisimamo na mabango nje ya Masjid Irshad, Chihota, Tandika, Dar es Salaam baada ya Swala ya Ijumaa, kuwakumbusha Ummah wa Kiislamu jukumu la kuinusuru Gaza na Masjid Aqswa.

